

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA TATU

15 SEPTEMBER, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA TATU – TAREHE 15 SEPTEMBER, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Maelezo ya Waziri wa Maji kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 [*The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 [*The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022*].

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

39. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Halmashauri katika Kata ya Nzera.

40. MHESHIMIWA NORAH WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Wodi za Wazazi nchini pamoja na kuongeza huduma hizo kwa Wananchi.

41. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Kagera/Nkanda Wilayani Kasulu.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

42. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, nini sababu ya kukosekana uwiano wa jinsia ya Kike kwenye nafasi za uteuzi na ajira.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:



43. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Vitambulisho vya Taifa na vyeti vya kuzaliwa Wananchi wa Ololosokwan, Soitsambu na Enguserosambu.

44. MHESHIMIWA ABDULRAHMAN MWINYI MOHAMED (CHAMBANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Wananchi wa Wilaya ya Mkoani waliosajiliwa kwa muda mrefu watapewa Vitambulisho vya NIDA.

45. MHESHIMIWA MAULID SALEH ALI (WELEZO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia Hati za Kusafiria kwa Wakandarasi wanaoingia nchini kutekeleza miradi mbalimbali.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

46. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-


Je, nini mpango wa Serikali kueneza matumizi ya TEHAMA katika kufundisha ili kuwaokoa Walimu na matatizo ya Mgongo na Shingo.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

47. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya zege ya Kilometa 3 kwenye Mlima Magara katika Jimbo la Mbulu Mjini.



IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 [*The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022*].

**DODOMA
15 SEPTEMBER, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**